**MAKALA**

# Mabadiliko ya sekta ya sheria: Nguzo muhimu ya Dira ya Maendeleo 2050

186590



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (katikati walioketi) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mara baada ya hafla ya utiaji saini Sheria zilizofanyiwa Urekebu iliyofanyika Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma tarehe 23 Aprili, 2025.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe, Hamza S. Johari akito huduma ya Ushauri wa Kisheria kwa Mwananchi wakati wa Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya na Kliniki ya Sheria bila malipo, tarehe 19 Mei, 2025 katika Viwanja vya Stendi ya zamani Manispaa ya Singida.

Wakati nchi ikijiandaa kuanza utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2050 kuanzia Julai mwakani, sekta ya sheria inaendelea kupitia mageuzi makubwa, yakijijenga si tu kama msingi wa utawala bora na pia kujenga jamii na uchumi imara, bali pia moja ya nyenzo za utekelezaji wa Dira hiyo. Kutoka kwenye matumizi ya teknolojia na upatikanaji wa haki hadi ukuaji wa taasisi, ufanisi wa kifedha na uongozi wa kikanda - taarifa za hivi karibuni zinaonyesha mfumo wa sheria unaoacha uendeshaji wa kizamani na kuwa mfumo wa kisasa unaotumia teknolojia kama injini ya kutoa huduma kwa umma.

**Mageuzi ya kihistoria**

Katika kile ambacho wataalamu wa sheria wanakiita mafanikio ya kihistoria, serikali ilikamilisha uchapishaji wa Toleo la Marejeo la Sheria za Tanzania la mwaka 2023, ambalo linajumuisha na kutafsiri sheria kuu 446 kwa lugha ya Kiswahili - lugha rasmi ya taifa. Jambo hili ni geni kwani imeshazoeleka nchini kuwa sheria zinaandakiwa kwa lugha ya Kiingereza.

Toleo hili jipya la sheria za nchi, ambalo lilianza kutumika rasmi Julai 1, 2025, ndilo la kwanza kuandikwa kwa gharama za serikali bila msaada kutoka Benki ya Dunia au wafadhili wa nje kama ilivyozoeleka. Umuhimu wa jambo hili ni kuwa toleo hilo jipya la sheria linatoa nafasi ya demokrasia ya kisheria kwa wananchi wengi, ambao sasa wanaweza kuelewa sheria kupitia lugha wanayoifahamu vema.

"Umiliki wa sheria huanza na lugha. Hii itasaidia kupunguza pengo kati ya sheria na wananchi," anasema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, aliyesimamia mchakato huo Kuanzia 2021 hadi 2025, Tanzania pia imetunga au kurekebisha sheria kuu 57 na zaidi ya nyaraka 4,000 za kisheria, jambo lililoboresha mfumo wa sheria katika maeneo kama fedha, mazingira, ardhi na uchumi wa kidijiti.

**Teknolojia na upatikanaji wa haki**

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, iliyoanzishwa chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, ni mojawapo ya nguzo za mabadiliko haya. Chini ya kampeni hii vituo vya msaada wa kisheria vilianzishwa katika mikoa 25. Vituo hivi vimewasaidia moja kwa moja watu milioni 2.7, huku zaidi ya watanzania milioni 6.4 wakipata elimu ya sheria kupitia mikutano na majukwaa ya umma.

Wakati huo huo, ushirikiano wa Tanzania na taasisi ya Laws. Africa na GIZ uliwezesha kuzifanyia mabadiliko makubwa asilimia 40 ya sheria ambazo sasa zinaendana na teknolojia ya kidijiti. Kazi hii ilifanyika hadi mwisho wa 2023 kupitia jukwaa la Indigo. Maelfu ya sheria hizo, pamoja na hukumu za mahakama, sasa zinapatikana bila malipo kupitia Tanzania Legal Information Institute (TanzLII).

Ilipangwa kuwa hadi kufikia Juni 2025, TanzLII iwe imechapisha hukumu 65,815 ili kuvutia watumiaji milioni 2.6. Mabadiliko haya hayajaleta mafanikio ndani ya nchi pekee. Kwa upande mwingine yamezivutia nchi nyingine za Afrika - maofisa kutoka Ghana na Nigeria walitembelea Tanzania mwezi Juni 2025 kujifunza mfumo huo.

**Ujenzi wa miundombinu ya sheria**

Mageuzi ya sheria yanaambatana na uwekezaji wa moja kwa moja katika miundombinu na rasilimali watu. Takwimu zilizopo zinaoneysha kuwa idadi ya majaji imeongezeka kutoka 92 mwaka 2021 hadi 146 mwaka 2025 huku idadi ya mahakimu nayo ikipanda kutoka 1,412 hadi 1,426.

Aidha, ujenzi wa vituo sita vya Haki Jumuishi (IJCs) umekamilika katika miji kama Dodoma na Mwanza, huku vituo tisa zaidi vikiwa katika hatua mbali mbali za ujenzi. Sambamba na hatua hiyo, mahakama nyingi za wilaya na msingi zimejengwa au kuboreshwa, hasa vijijini. Hatua hizi zimepunguza mrundikano wa kesi, kuboresha upatikanaji wa haki na kuiweka Tanzania katika nafasi ya uongozi wa maendeleo ya miundombinu ya haki katika ukanda huu.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe.Hamza S. Johari

**Mafanikio yaokoa fedha**

Nje ya mahakama, taasisi za kisheria pia zimeleta faida kubwa kifedha. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ilitatua kwa mafanikio kesi 966 zikiwamo 814 za ndani na moja ya kimataifa na kuokoa kiasi cha TSh bilioni 232.7 (zaidi ya dola milioni 100), ambazo zingetumika iwapo kesi hizo zingeendeshwa kwa mfumo wa kawaida.

Haya ni matokeo ya mikakati bora ya kupunguza hatari, ushauri wa mapema wa kisheria na taaluma bora ya mawakili wa serikali wanaopatiwa mafunzo chini ya mpango mpya wa "Legal Excellence for Tomorrow". Mpango huo pia unahusisha uanzishwaji wa mfumo mpya wa Usimamizi wa Kesi (CMIS), maktaba ya sheria mtandaoni na tovuti ya kisasa ya mawakili wa serikali.

**Uongozi wa kikanda**

Mafanikio ya Tanzania katika sekta ya sheria yanazidi kutambuliwa na nchi nyingine barani Afrika. Mbali na kupokea wageni kutoka Afrika Magharibi, nchi pia inaongoza mijadala ya bara kuhusu upatikanaji wa sheria kwa uwazi, mifumo ya kidijitali ya mahakama na haki kwa wote.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Ally Possi, wameunganisha juhudi za kisasa za sheria na Dira ya Maendeleo 2050, wakihimiza wataalamu wa sheria kuonisha mifumo ya kisheria na malengo ya taifa kama vile uanzishaji wa viwanda, kuvutia uwekezaji na kukuza uchumi wa kidijitali. "Sekta ya sheria lazima iwe kitovu cha maendeleo ya taifa - si pembeni," alisisitiza Johari kwenye mkutano wa kikanda huko Arusha.

**Kwa nini ni muhimu**

Mabadiliko haya hayahusu mahakama pekee, bali yanahusisha ujenzi wa mfumo wa sheria unaolinda haki, kuvutia wawekezaji, kujenga imani ya wananchi na kuhimiza maendeleo jumuishi. Kwa wafanyabiashara, hii inamaanisha sheria zilizo wazi, utatuzi wa migogoro kwa haraka na mazingira yanayotabirika.

Hali hii inachochea sana uwekezaji na biashara kutoka nje ya nchi. Kwa wananchi, inamaanisha kuwa sasa watakuwa wanapata haki karibu na mahali wanapoishi. Hawalazimiki tena kusafiri umbali mrefu kutafuta haki zao. Kwa Bara la Afrika, Tanzania inazidi kuwa mfano wa mageuzi ya sheria yaliyojengwa kwa lugha ya wananchi, yanayoendeshwa na teknolojia, na yanayoleta matokeo kwa jamii. Kadri Dira ya Maendeleo 2050 inavyopiga hatua, sekta ya sheria inaweza kuwa injini tulivu ya mafanikio hayo - ikiweka viwango vya uwazi, usawa na ufanisi katika utawala na usimamizi wa maendeleo ya kiuchumi